SERA YA UADILIFU WA BIASHARA NA VIWANGO VYA UTENDAKAZI

Wastani na Mwongozo

AngloAmerican

UTANGULIZI

Uadilifu na uwajibikaji ni maadili makuu ya Anglo American. Mapato na kuendelea kuaminika ni muhimu katika ufanisi wa biashara yetu. Washikadau wetu wanafaa kuwa jasiri kwamba tutawashughulikia bila mapendeleo na kwa kufuata maadili yaliyowekwa.

Kanuni Zetu Nzuri za Biashara ya Uraia (hapa inarejelewa kama Kanuni Za Biashara) zimeweka wazi viwango ambavyo vinatuongoza katika kufanya biashara zetu. Zinafanya mambo kuwa wazi ya kwamba tunapinga vikali ufisadi. Hatutatoa wala hatutakubali hongo na hata kuwaruhusu wengine kufanya hivyo kwa jina letu, ama katika shughuli zetu na ofisa wa umma au na wagavi na wateja. Tumejitolea kutumika katika viwango vilevile vya juu vya uadilifu popote tufanyapo kazi.

Tukiwa wawekezaji wa muda-mrefu, tumejitolea katika kuchangia kwenye maendeleo endelevu na utawala bora wa nchi ambazo tunafanyia kazi. Ufisadi unapuuza lile lengo; unaondoa imani, unafukuza uwekezaji, unapuuza sheria ya kanuni ambayo usalama wetu wa uwekezaji unategemea, na unaongeza gharama na hali ya kutojua matokeo ya biashara tunazofanya. Unapunguza kwa kiwango kikubwa uwezo wa biashara yetu katika kuzalisha matokeo mazuri ya maendeleo.

Hongo na malipo ya ufisadi ni haramu. Kwa kuongezea kukubaliana na sera hii, wafanyakazi i wetu na wakandarasi wanalo jukumu la kushikilia na kukubali sheria za nchi pamoja na mamlaka ambayo wanafanyia kazi.

Kusudio la sera hii ni kuweka wazi viwango vinavyohitajika vya kufanyia kazi katika kila daraja ndani ya Anglo America, matawi yetu, washiriki ubia na wasaidizi; kwa sehemu nyingine wale ambao tunafanya biashara nao na wale ambao wanafanya kazi kwa niaba yetu, katika kukabiliana vikali na tabia ya ufisadi wa kila aina.

Viwango vya Utendakazi Vinavyolenga katika Kukabiliana na Ufisadi (hapa vinarejelewa kama Viwango vya Utendakazi) vimeweza kuanzishwa ili kusimamia sehemu zifuatazo na vinapatikana pindi vitakapohitajika kutoka katika idara ya Ukubalifu wa Uadilifu wa Biashara.

A – Zawadi, burudani na ukarimu

B – Mgongano wa mahitaji

C – Malipo ya kusahilisha

D –Matumizi ya rasilimali ya kampuni

E – Msaada wa kisiasa

F – Utangamano na maofisa wa serikali pamoja na utetezi

G – Msaada wa wema

H – Jamii na Uwekezaji katika jamii na shughuli za maendeleo ya kampuni

I – Ufadhili

J – Kuhifadhi na malipo ya wenzetu

K – Wanamseto, uchukuzi, ushiriki bia na wasaidizi

Tumejitolea, kupitia katika kujishirikisha kwetu kwenye mipangilio ya kimataifa kama vile uanzishaji wa Viwanda vya usindikaji (Ari) moyo wa kuanzisha uwazi(EITI), katika kufanya kazi na washikadau serikalini, biashara na vyama vya kiraia ili kuendeleza utawala bora, matumizi bora ya utajiri wa madini na uzuiaji wa ufisadi. Tutaweza kutetea vikali EITI katika nchi ambazo tunafanyia kazi. Katika zile nchi ambazo serikali iliyotukaribisha imeamua kutekeleza mpango wa EITI tutawaunga mkonokwa dhati katika shughuli hiyo. Kwa kuongezea hayo, tutaweka wazi malipo yetu ya ushuru kwa nchi zetu karibu zote tunapofanya kazi i kwenye 'Ripoti kwa Jamii' ya kila mwaka.

UTANGULIZI

UFISADI NI NINI?

Kwa kusudio la sera hii, ufisadi unatafsiriwa kama kitendo chochote kinachonuia katika kusababisha matumizi mabaya ya mamlaka uliyopewa kwa manufaa ya kibinafsi au ya kikampuni. Ufisadi unajumuisha mseto wa hali zinazojumuisha hongo, migongano ya mahitaji, wizi, upokonyaji, ubadhirifu, ulaghai na matumizi mabaya ya rasilimali za kampuni.

Utoaji hongo unatafsiriwa kama kuahidi, kutoa au kupatia manufaa yasiyostahili kwa mtu au kampuni, ama moja kwa moja ama kupitia kwa mtu mwengine, ili mtu huyo au kampuni hiyo iweze kutekeleza, au kujizuia kutenda, kitendo ambacho kitakuwa kinavunja sheria za biashara zao au majukumu ya umma. Mifano maarufu ya utoaji hongo ni pamoja na:

- pesa au njia nyingine za malipo ili kujipatia kandarasi au kupata leseni
- utoaji misaada isiyofaa kwa vyama vya kisiasa au mashirika husika; na
- utoaji zaidi wa zawadi au burudani inayonuia katika kuathiri yule mpokezi ili atekeleze hatua fulani inayohitajika.

Kwa kusudio la sera hii, hongo inaweza kuwa kituchochote chenye thamani , na si tu malipo kwa pesa taslimu, na huenda pia ikajumuisha utoaji au upokeaji wa:

- zawadi za kupendeza zisizoeleweka kwa nini zimetolewa na burudani
- misaada kwa njia isiyoeleweka
- malipo ya gharama za usafiri au malazi kwa mteja au ofisa pale ambapo hakuna kusudio lolote la biashara katika ziara hiyo; au
- Matumizi ya rasilimali za kampuni kwa shughuli ambazo hazihusiani na biashara yetu au makusudio yaliyoidhinishwa katika msaada huo.

Migongano ya mahitaji inaweza kutokea pale ambapo marejeleo ya kifedha au ya kibinafsi huenda ikaathiri au ikaonekana kuathiri uamuzi au vitendo vya wafanyakazi wetu katika kutekeleza majukumu yao, au uwezo wakufanya hivyo. Migongano kama hiyo inaweza ku kutokea pale ambapo mahitaji ya kibinafsi au ya kikampuni huchanganyika au pale ambapo biashara au uamuzi wa kiserikali huwa ni kwa mujibu au mahitaji ya kibinafsi.

Kupokonya hutafsiriwa kama matumizi ya kiharamu ya nafasi rasmi au mamlaka ya kuweza kupata mali au fedha.

Ulaghai unaweza kutafsiriwa kama uongo wowote unaofanywa kwa makusudi ili kuweza kujipatia manufaa ya haramu au yasiyo halali kisheria..

Shughuli ya hatari isiyofaa

Hatutawahi, ama moja kwa moja ama kupitia kwa mtu mwingine au mtu au wahusika, kuomba, kupokea, kutoa, kuahidi au kupatia pesa au kitu chochote chenye thamani ya mali (ikiwa ni pamoja na taarifa ya faragha au nyeti ya kibiashara na kifedha pamoja na rasilimali za kiakili) au vinginevyo kufanya athari isiyofaa katika biashara yetu au uhusiano wetu wa kiserikali, kwa nia ya kupata kandarasi, ruhusa au manufaa yoyote mengine mahsusi au faida isiyo rasmi katika kuendesha biashara.

Hii inatumika kotekote katika uhusiano wetu na mashirika ya kiserikali na hata katika shughuli zetu na biashara nyingine au mashirika mengine ya kiraia. Hatutaweza kuvumilia shughuli nyingine kama hiyo kutoka kwa wafanyakazi wetu, wakala, wkandarasi(watoaji huduma) au washiriki wa biashara.

Swali la ni nini kinachofanya ‘thamani ya mali’ hutegemea na muktadha. Itatafsiriwa na:

1. Muktadha wa uwezekano wa kushurutishwa, na
2. Kama kile kinachotolewa au kuahidiwa kinao uwezo wa kuwa na thamani tosha kwa yule mpokeaji, ama kifedha au kwa hali tu yake, ili kuwa na uwezo wa maoni ya yule mpokeaji au vitendo.

Sera hii inahusu kule kuomba na kupokea hongo au vishawishi vingine kutoka kwa watu wengine na wafanyakazi wa Anglo American pamoja na utoaji wa malipo ya hongo.

UTENDAKAZI MAPITIO YA– VIWANGO

Viwango vya Utendakazi vinanuiwa kuwa muongozo katika kusaidia kutambulisha na kufasili hali za ufisadi wenyewe au uwezekano wa ufisadi. Viwango ni kanuni ambazo zinalenga na zinazotoa mpangilio ambao wafanyakazi wanatarajiwa kufanya uamuzi wao bora zaidi kwa kuhusiana na hali mahsusi.

Viwango Hivi vya Utendakazi vinatumika kwa wafanyakazi wote wa Anglo American na watoaji huduma. Kandarasi za mtoa huduma (mgavi) wa Anglo American zitahitaji wagavi wa bidhaa na huduma kwa Kampuni kufuata sera hii au viwango kama hivi na wawakilishi wa Kamati yetu watajitahidi kuhakikisha ufuatiliaji i wa viwango fananishi katika shughuli zetu za pamoja au za kampuni saidizi.

UTANGULIZI

A – ZAWADI, BURUDANI NA UKARIMU

Utoaji au upatianaji wa zawadi, burudani na ukarimu

Ubadilishanaji wa zawadi nzuri na burudani huenda ukasaidia katika kujenga uhusiano na sera hii hailengi katika kuzuia swala hili la kutamanika ambalo linalenga katika kuendeleza uhusiano mzuri kati ya washiriki wa biashara na washikadau wengine kupitia katika utangamano wa halali, wa mara kwa mara na wa kijamii.

Hata hivyo, utoaji au upatianaji wa zawadi zisizofaa au burudani huenda kukasababisha aibu kwa Anglo America na ukaharibu sifayetu. Malalamiko fulani hutokea pale ambapo ule utoaji wa zawadi na burudani huenda ukawa na uhusiano kwa njia moja na shughuli ya biashara halisi au uwezekano huo au hata katika kuiidhinisha. Hata kama nia si ufisadi, bado kuna hatari kwamba mpokeaji au mtu mwingine mwenye nia kama hiyo huenda akapokea zawadi au burudani hiyo na akaona na akajaribu kupata faida isiyofaa.

Zawadi yoyote au burudani kila wakati haitakubalika kama:

- inatolewa au kufanywa ili kuwe na mbadilishano wa kandarasi, kibali au faida yeyote nyingine mahsusi
- inatolewa ili kupata manufaa yasiyofaa katika shughuli ya biashara
- haiingiliani na sheria za nchini au za kimataifa kuhusu hongo
- itachukuliwa kama isiyokubalika kama itatolewa na mgavi au mshiriki wa biashara kwa mmojawapo wa wafanyakazi wetu; na
- itaweza, kama itafanywa kuwa ya umma, huathiri vibaya jina letu.

Kupokea zawadi, burudani na ukarimu

Tunalo jukumu la kuhakikisha kwamba shughuli zetu na wagavi ni kwa mujibu wa uamuzi wa malengo na hatuathiriki na zawadi au vibali. Tunazuia wafanyakazi katika kuomba au kupokea zawadi na burudani ikiwa pamoja na fadhilai, bidhaa, kiinua mgongo, pesa na huduma ambazo:

- huenda zikaleta hisia za kuwajibika
- Huenda zikaathiri au zikaonekana kwamba zinaathiri uamuzi wao wa biashara; au
- Huenda zikaleta, au ikaonekana kuleta, mgogoro kati ya mahitaji ya kibinafsi ya mfanyakazi na yale ya mwajiri wake au kundi la Anglo America kwa ujumla.

B – MIGOGORO YA MAHITAJI

Wafanyakazi lazima waepuke migogoro halisi au inayoonekana kwa mujibu wa mahitaji yao, kujihusisha au kuhusisha ndugu zao wa karibu na pale ambapo mgogoro kama huo unao uwezo wa kutokea i lazima wafahamishe msimamizi wa idara yao na mtu mwingine ambaye ameruhusiwa na Kitengo chao cha Biashara au kampuni husika kwa kusudio hili.

C – MALIPO YA KUSAHILISHA

Tunazuia ile hali ya kusahilisha malipo. Malipo ya kusahilisha ni malipo ya thamani halisi yanayotolewa kwa ofisa wa kiwango cha chini wa serikali ambaye majukumu yake hususan ni ya kiutawala ili kuweza kuhakikisha utendakazi wa hatua za kila siku za kiserikali ambazo yule mlipaji-anastahili kuzipata kisheria. Mifano ya malipo kama hayo ni kama vile malipo ya kushughulikia maombi ya visa au kuunganisha umeme au ugavi wa maji, pale ambapo mahitaji yote yanayofaa yametimizwa tayari.

Tunatambua kwamba mara kwa mara malipo huwezakudaiwa kwa kitisho . Kitisho inaweza kutafsiriwa kama ile hali ya vurugu halisi au vurugu ya kutishia, kufungwa jela au tishio jingine la kibinafsi la kushirikiana na mtu katika kuingia kwenye mkataba au kufanya kitendo dhidi ya mahitaji yao. Tishio linaweza kuwa kwa watu wenyewe au kwa watu wengine. Hatutarajii wafanyakazi wowote kuweza kuhatarisha usalama wao au ule wa wengine ili kukubaliana na sera yetu, lakini tunahitaji wafanyakazi kuweza kupiga ripoti ya tukio lolote pale ambapo wametishiwa au wamedharauliwa ili hatua inayofaa iweze kuchukuliwa kuzuia hali nyingine kama hiyo.

D – MATUMIZI YA RASILIMALI ZA KAMPUNI

Hatutawahi, ama moja kwa moja au kupitia kwa wenzetu na watu wengine wa kando, kutoa, kuahidi, au kupatia pesa au kituchochote cha thamani au vinginevyo kusababisha athari isiyofaa katika uhusiano wetu wa biashara, kwa nia ya kupata kandarasi, kibali au manufaaa yoyote mengine mahsusi au kupata ubora wowote usiofaa katika shughuli ya biashara. Hii inatumika kote katika uhusiano wetu na mashirika na maofisa wa serikali na hata katika kushughulika kwetu na sekta ya kibinafsi. Hatutavumilia shughuli nyingine kama hii kutoka kwa wafanykazi wetu au washiriki wa biashara.

Matumizi ya rasilimali ya kampuni kama vile ofisi, mitambo au magari, bure bila malipo inawakilisha kitu cha thamani kwa mpokezi aliyenuiwa. Rasilimali za kampuni hazifai kutolewa kwa matumizi ya kibinafsi au matumizi ya kipekee kwa wateja, ofisa wa umma au watu wengine pale ambapo hakuna kusudio lolote halisi la kibiashara au manufaa wazi ya umma hayajaonekana.

E – MISAADA YA KISIASA

Tunazuia utoaji wa misaada kwa makusudio ya kisiasa kwa mwanasiasa yeyote, chama cha kisiasa ama shirika husika, ofisa wa chama cha kisiasa au mgombeaji wa ofisi ya kisiasa katika hali yoyote ama moja kwa moja ama kupitia kwa watu wengine.

F – UTANGAMANO NA OFISA WA KISERIKALI NA USHINIKIZAJII

Tunaendeleza uaminifu na ushirikishwaji unaofaa na serikali yetu mwenyeji katika viwango vyovyote. Tunashauriana pakubwa na watu ambao wameathiriwa na shughuli zetu na tutaendelea na shughuli zetu pamoja na serikali na maofisa wa umma katika njia za uwazi na kimaadili.

Hatutawahi, ama moja kwa moja au kupitia kwa wenzetu na watu wengine, kutoa, kuahidi au kupatia pesa au chochote chenye thamani ya kushikika au vinginevyo au kutafuta athari isiyofaa katika uhusiano wetu wa biashara, kwa kusudio la kupata kandarasi, kibali au manufaa yoyote mengine mahsusi au ubora usiofaa katika kufanya biashara. Hii inatumika kote katika uhusiano wetu na mashirika na maofisa wa serikali na katika shughuli zetu na sekta ya kibinafsi. Hatutavumilia shughuli yoyote ya wafanyakazi wetu au washiriki wa biashara.

UTANGULIZI

G & H – MISAADA YA WEMA NA UWEKEZAJI KATIKA JAMII NA MAENDELEO YA SHUGHULI ZA BIASHARA

Tunatoa michango ya wema na ya kijamii na uwekezaji wa jamii kwa lengo la kuendeleza maendeleo ya jamii endelevu, kukabiliana vikali na umaskini na ugonjwa, kulinda mazingira na kuendeleza uwezo wa watu au taasisi katika nchi ambazo tunafanyia kazi. Tunatunza, hata hivyo, ufadhili kama huo haufanyi kazi kimsingi katika kufaidisha ofisa fulani wa serikali , mwanasiasa au chama na huwa tunaweka vidhibiti mahali pake katika kuhakikisha kwamba havitumiwi vibaya na watu wengine. Michango na uwekezaji wa kijamii na jamii haifai kutolewa kama italeta au itakuwa na uwezo wa kuleta utambuzi wa kutowajibika.

Katika shughuli zetu kwa jamii na wakilishi wao tutaweza kutenda kwa uwazi na kwa nia njema.

I – UFADHILI

Ufadhili huenda usiahidiwe, kutolewa au kupatiwa katika kubadilishana na kandarasi, kibali au manufaa mahsusi ya utendakazi. Haufai kutolewa ili kupata faida isiyofaa katika kufanya biashara au kama huenda ikaonekana kutambuliwa kama kuwa na nia hii.

J & K – UHIFADHI NA ULIPAJI WA WATU WENGINE WA KANDO NA WANAMSETO, UCHUKUZI, USHIRIKI BIA NA WASAIDIZI

Jina letu linaweza kuharibika kutokana na hatua za watu wengine kama vile washauri wagavi, wakala, watoaji huduma, watetezi na washiriki wa kufanya kazi kwa pamoja na Anglo American huenda ikajipata ikiathirika kwa hatua zao. Haikubaliki kwa mtu mwengine kuweza kutekeleza kitendo kwa niaba ya Anglo American ambapo, kama ingefanywa na Anglo American moja kwa moja, kungekuwa na mvunjiko wa sera hii.

Ili kulinda dhidi ya hatari ya hongo zinazotolewa kwa njia za pembeni, tumejitolea katika:

- kufanya hatua zote zinazowezekana katika kuhakikisha kwamba washiriki wetu wa biashara wanaelewa na kukubaliana na Viwango na Sera ya Uadilifu wa Biashara na Viwango vya Utendakazi vya Kuzuia rushwa
- uchunguzi wa heshima na sifa za washiriki wetu wa biashara na utekelezaji rasmi , pale inapofaa, kujitosheleza sisi wenyewe katika uadilifu wetu na uadilifu na ukweli
- kuweka mahali pake vidhibiti vinavyofaa na vionyeshi vya kufuatilia matumizi ya pesa za Anglo American na mtu mwingine anayedai kufanya kazi kwa niaba yetu; na
- kuhakikisha kwamba ushiriki bia na kampuni saidizi zinazo shughuli kama hizo ambazo zinaeleweka.

Tumejitolea katika kufanya uchunguzi kabisa wa hali ya mambo, sifa, kimaadili na hata faida za kitamaduni za kampuni yoyote ambayo tunawekeza ndani au tunamiliki na mshiriki yeyote ambaye tunaamua kuingia katika ushirikiano wa pamoja naye, na ile hali ya uwekezaji ambayo sote tunarithi.

MWONGOZO NA UPIGAJI RIPOTI

Ufisadi huja kwa njia mbalimbali. katika mifano mingi njia halisi ya kuchukua hatua huenda isiwe wazi siku zote. Wafanyakazi lazima waombe ushauri na kushauriana kama hawana uhakika kuhusu hali halisi ya kufanya.

Usalama wa watu wetu

Wafanyakazi wa Anglo American wanafaa kuwa huru kutekeleza majukumu yao bila ya uoga au kutishiwa kwa vurugu. Usalama na ulinzi wa wafanyakazi wetu ndilo hitaji letu kuu. Hatutarajii wafanyakazi wetu kujihatarisha kuwa salama au kupata usalama wao au kwamba ule wa wengine ili kukubaliana na kanuni za sera hii.

Wafanyakazi wanafaa, hata hivyo, kupiga ripoti mara moja kuhusu tukio lolote pale ambapo wametishiwa au wamelazimishwa kufanya kazi au kitendo ambacho huenda kikasababisha mvunjiko wa sera hii kwa yule mtu ambaye ilinuiwa ndani ya Kitengo cha Biashara, iliyonakiliwa katika Idara ya Ukubalifu wa Uadilifu wa Biashara. Baada ya ushauriano unaofaa wa ndani matukio kama haya yafaa kupigiwa ripoti kwa mamlaka inayohusika ili kuzuia kutokea tena.

Uvunjaji wa sera hii

Wafanyakazi lazima wapige ripoti kuhusu uvunjaji wowote, au uwezekano wa uvunjaji wa sera hii, pindi watapojua. Ukiukaji wa sera hii utasababisha hatua ya kinidhamu kulingana na taratibu za nidhamu za Kundi ikiwa pamoja na Sera kuhusu Makosa ya Biashara. Hatua za kinidhamu huenda zikahusisha vikwazo vya kiuchumi na pamoja na muhtasari wa kuachishwa kazi Tumejitolea katika kupiga ripoti matukio yote ya ufisadi na mbinu nyingine za udanganyifu kwa mamlaka husika na kutekeleza hatua ya kihalifu dhidi ya mtu(watu) wanaohusika na tutatafidia hasara yoyote itakayotokana na hatua kama hii.

Ongea

Huduma ya ongea inatoa hali ya ufaraga na usalama kwa wafanyakazi wetu, watoaji huduma, wagavi, washiriki wa kibiashara na washikadau wengine wa nje kupiga ripoti na kutoa malalamiko kuhusu jinsi ambavyo tunafanya kazi kinyume cha maadili yetu na viwango, kama vilivyofafanuliwa katika Kanuni zetu za Biashara, Sera ya Uadilifu wa Biashara na Viwango vya Utendakazi vya Kuzuia Ufisadi.

Ongea hutoa mawasiliano yanayotolewa kwa njia ya simu, kwa baruapepe na tovuti na yanayosimamiwa na kampuni huru katika maeneo ambayo Anglo American hufanyia kazi. Huduma inapatikana masaa 24 kwa siku, siku saba kwa juma na hujumuisha pia huduma za tafsiri. Kiungo cha huduma ya Ongea kinatolewa katika Shina/ rejeo. Unaweza kuwasiliana na ONGEA pia kupitia kwa www.anglospeakup.com au kwa kutuma baruapepe anglocorp@anglospeakup.com.

Anglo American haitavumilia namna yoyote ya kulipiza kisasi dhidi ya wafanyakazi wanaozua malalamiko kwa nia safi Madai ya kulipiza kisasi dhidi ya unyanyasaji au utishwaji wa mfanyakazi na watu wengine kutokana na mwito wa ONGEA Yatachunguzwa na hatua inayofaa kuchukuliwa, ikiwemo hatua ya kinidhamu hadi kufikia na kujumuisha kuachishwa kazi kwa mfanyakazi ambaye amepatikana na hatia hiyo.

Cynthia Carroll
Ofisa Mkuu, Anglo American plc

Uadilifu wa Biashara ya Anglo American
Idara ya Ukubalifu
20 Carlton House Terrace
London
SW1Y 5AN
T +44 (0) 20 7968 8946
E lthorne@angloamerican.co.uk

www.angloamerican.com

MEI 2011

Sera hii itakuwa inaangaliwa upya katika wakati unaofaa na kudurusiwa pale itakapohitajika ili iende na wakati.